OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.
MKOA WA NJOMBE
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE

SHULE YA SEKONDARI LUPILA,
S.L.P. 602,
**NJOMBE.**
29/03/2022

KUMB. NA. LSS/JI/78/50.

24/04/2020 NDUGU MZAZI/MLEZI WA …………………………………………. ………………………………………….

YAH: <u>KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022/2023</u>

1<u>. UTANGULIZI</u> Ninayo furahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano katika shule ya sekondari Lupila kulingana na chaguo lako___________

Shule itafunguliwa tarehe ……/……/2022, shule yetu ina tahasusi (Combinations 3) **HKL, HGK na EGM**. Shule ipo wilaya ya Makete Mkoa wa Njombe, KM 76 kutoka Makete mjini na KM 100 kutoka Njombe standi kuu ya mabasi. Usafiri wa mabasi upo kila siku kuanzia Njombe standi kuu ya mabasi hadi Lupila kwa Tsh 10,000 na muda ni saa 6:00 mchana kwa mabasi ya kampuni ya MPAMBALYOTO COACH. Usafiri kutoka Makete mjini kupitia Ikonda kwenda Lupila siyo wa uhakika labda kama una usafiri binafsi. Ukifika lupila kituo cha Idangaja usafiri wa bodaboda upo kwa Tsh.2000.

2. <u>MAHITAJI</u>

A. FEDHA

i) ADA ya shule sh. 70,000/= kwa mwaka au Tshs.35,000/= kwa muhula kadiri ya uwezo wa mzazi.

ii) Mchango wa Taaluma Tsh. 20,000/=

iii) Ukarabati wa samani Tsh. 20,000/=

iv) Wapishi,Ulinzi na Matron Tsh. 30,000/=

v) Huduma ya kwanza hapa shuleni (FIRST AID) Tsh. 12,000/=

vi) Kitambulisho Tsh. 6,000/=

vii) Fedha ya Tahadhari Tsh5,000/= (haitarejeshwa)

viii) Umeme Tsh 20,000/= (Umeme wetu ni wa mfumo wa jua ambao unahitaji marekebisho ya mara kwa mara)

ix) UMISETA Tsh 5000/=

x)

**MUHIMU**: Jumla ya ada na michango kwa mwaka mzima ni Tsh. = 188,000/=.

Michango yote inatakiwa ilipwe awamu ya kwanza, isipokuwa ada inaweza kulipwa nusu au yote. Ambayo jumla yote ukilipa ada nusu itakuwa Tshs.153,000 /=.



Edit with WPS Office

FEDHA HIZI ZOTE ZILIPWE BENKI (NMB 60410010351 SHULE YA SEKONDARI LUPILA)

Andika jina la mwanafunzi unayemlipia na orodhesha vitu vilivyolipiwa. Hatutapokea fedha. Njoo na BPS (BANK PAY SLIP OR HATI YA MALIPO YA BENKI) hapa shuleni na utakatiwa risiti.

B. VIFAA VYA USAFI: kila mwanafunzi aje na vifaa kwa ajili ya usafi wa mazingira ya shule kama ifuatavyo; JEMBE LENYE MPINI 01, SOFT BROOM 01, HARD BROOM 01, MOPPER 02, TOILET BRUSH 01, CHELEWA KUBWA 02 NA KWANJA 01.

4. SARE ZA SHULE (WASICHANA)

1. Suruali 01 (damu ya mzee) na Sketi moja rinda box rangi ya chocolate inayo gusa visigino.
2. kigauni cheupe mshono wa solo kitambaa(pamba nyeupe) kimoja (01) na shati mikono mirefu 01
3. Sweta 02, (damu ya mzee)
4. Jezi za michezo rangi nyekundu au blue na raba za michezo jozi moja. Michezo ni ya lazima.
5. Viatu vya ngozi jozi mbili rangi nyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu.
6. Soksi jozi mbili ndefu nyeupe.
7. Track suit moja ya blue au nyeusi itavaliwa wakati wa usiku (night preparation).
8. Jacket moja zito jeusi lenye kofia lisilo na maandishi yoyote kwa ajili ya baridi, majaketi marefu yanayovuka magoti hayaruhusiwi kabisa.
9. Pull neck nyeusi (kabashingo).
10. Kwa wanafunzi wa kiislamu waje na hijabu nyeupe kwa ajili ya kuvaa darasani wakati wa vipindi na dark blue hizo zitavaliwa na shamba dress.
11. Shamba dress dark blue inovuka magoti.
12. T-shirt inapaitkana shule kwa tsh 15,000/=
13. Njoo na barakoa zinazoweza kufuliwa zisizopungua 05 kwa ajili ya kujikinga na COVID-19.

NB. SURUARI MOJA, SKETI RINDA BOX MOJA NA KIGAUNI KIMOJA SOLO UTASHONEWA UKIFIKA SHULENI KWA GHALAMA YA TSH 20,000/= KWA KILA KIMOJA NA JUMLA NI TSH 60,000/=

5. VIFAA VYA BWENI (WASICHANA)

a) Godoro la sponchi size ft 2 1/2 aje nalo.

b) Mashuka (2) rangi ya pinki, blanketi zito (kuna baridi) kanga au kitenge doti moja na taulo.

c) Vyombo vya kulia chakula bakuri lenye mfuniko, kijiko na kikombe.

d) Toilet paper, mafuta ya kupaka, dawa ya meno, miswaki na sabuni

e) Ndoo mbili za lita 10 zenye mifuniko.

f) Sanduku (Tranka) la kuhifadhia vifaa 1 na kufuli imara.

6. MAWASILIANO YA SHULE

a) Barua S.L.P 602, NJOMBE

b) SIMU YA SHULE 0754588298 kwa ajili ya mawasiliano yao na wazazi/walezi wao wanapokuwa na matatizo au kuomba fedha za matumizi. Namba hizi hutumika kwa mawasiliano na kutuma fedha (MPESA). Andika Jina la mwanafunzi unayemtumia, Na kidato chake.



Edit with WPS Office

MUHIMU:

1. Ni mwiko kwa mwanafunzi kumiliki **SIMU** au **LAINI** ya simu shuleni, Ni marufuku kuja na simu shuleni, simu shuleni hairuhusiwi.

7. VIFAA VYA KITAALUMA

I) Daftari counter books 10 kwa ajili ya notes za masomo yake (akiweza aje na fedha atapata hapa shuleni) school bag ni lazima kwa ajili ya kuhifadhia madaftari hayo.

II) Advanced Dictionary kwa wote

III) Wanaochukua Tahasusi yenye Kiswahili waje na kamusi na wanaochukua Tahasusi yenye Geography waje na Atlas.

IV) Ream A4 (Bunda (02)

ENGLISH LANGUAGE

a) James J (2012, Advanced English Language, form six and form five, Oxford university press.
b) Asheri N. (2010) Advanced level English Second Edition, Good book publisher, Dar-es-salaam.
Advanced literature

NOVELS

a) A man of the people – Chinua Achebe
b) The Rape of the pearl – Magala Nyajo
c) The Beautyful Ones are Not Yet Born- Ayi Kwei Amah

PLAYS

a) An enemy of the people – Henrick Ibsen
b) The bride – Austin Bukenya
c) I will Marry When I want- Ngugi Wa Thiong'o

POETRY

a) Selected Poems – Institute of Education
b) The wonderful surgeon and other poems – Charles Mloka.

VITABU VYA KISWAHILI

Kiswahili II

a) JPD Company (2008) Kiswahili II kidato cha 5 & 6 General supplies Ltd Dar es salaam. J.A. Masebo (2011) – b) Nadharia ya fasihi k. 5 na 6 Nyambari nyangwine.



Edit with WPS Office

ZIADA

a) Kaptura la Max – Kezirahabi

b) Rosa Mistika – Kezirahabi

c) Mirathi ya hatari –

d) Moto wa mianzi

e) Ngoma ya mianzi

f) Ngome ya mianzi

USHAIRI

a) Kimbunga – Haji Gora
b) Fungate ya Uhuru – Mapenzi bora – Shaban Robert
c) Chungu tamu – T. Mvungi

RIWAYA

**a)** Mfadhili – Hussein Tuwa

**b)** Kufikirika – Shabani Robert

**c)** Usiku utakapokwisha – Mbunda Msokile

**d)** Vuta n'kuvute – Shafi A. Shafi

TAMTHILIYA

a) Morani – Emmanuel Mbogo
b) Kivuli kinaishi – Said Mohamed
c) Nguzo mama – Penina Mhando
d) Kwenye ukingo wa thim –

KISWAHILI I

**a)** Saluhaya (2010) Nadharia ya lugha STC DSM – Tanzania Masebo J.A (2012)

**b)** Nadharia ya Kiswahili kidato cha 5 na 6 G/S FORM V & VI

**c)** Nyambari Nyangwine (2009) Advance Level General Studies notes Nyambari Nyanga

GEOGRAPHY

a) Clarke. J. T. (Ed) (1975) An Advanced Geography of Africa.
b) K.K. Sibugu & I.P. Isengum (1986) Outline of soil Science.
c) Msabila D.T. (2003), Success in Geography climatology
d) The Essential of practical Geography advanced level form 5 & 6. Notes, Qn with answers. (J.W.N and F.K. Salosu Jacob)

HISTORY I & II

**a)** Oxford (2011) Advanced learners. History form 5 and 6. Oxford university press (T) Ltd. Dar-es-salaam.



Edit with WPS Office

b) Kamili 2 (2015) Advanced level. History part one alive. Kot Dublishers.

c) Walter Rodney, (1976) how Europe underdeveloped Africa. TPH, DSM

d) Perry Davis, (1985) History of the world Houghton Milton Company Washington.

e) Modern world History Second Edition (Ben Wash)

f) World history modern Era (Ellis Esler)

g) Advanced History 1 and 2 by Sarehe Yasin

h) Advanced History 1 and 2 by Shibitali

UCHUMI

a) Odhiambo, A. (2019). Essentials for A-Level Economics Paper 1 Odhiambo ,

b) A. (2018). Essentials for A-Level Economics Paper 2

c) Kamili, Z. (2014). Economics 1

d) Kamili, Z. (2014). Economics 2

MATHEMATICS

a) Backhouse, J. K. (1985) Pure Mathematics 1, 4th Edition.LongmanGroup Ltd.

b) Hermes D. S. and Mosha, I (2019). Advanced mathematics 1&2 Review.

NB. Kitabu chochote cha kidato cha 5 na 6 kinacho faa unaweza kukinunua.

MUHIMU. KWA KILA MWANAFUNZI HAKIKISHA UNA VITABU VYA MASOMO YA TAHASUSI YAKO KWA AJILI YA KUJISOMEA.

SIMU ZA WALEZI WAO (WALIMU)

a) Mkuu wa shule - 0628043943/0764817475
b) Makamu mkuu wa shule – 0623797358/ 0719738191
c) Mhasibu wa shule - 0624708706
d) Malezi - 0623588743
e) Taaluma –0622646867

7. MAELEKEZO MUHIMU

a) Baadhi ya wazazi wamekuwa na tabia ya kutelekeza watoto wao bila kuwapa mahitaji muhimu na fedha za matumizi wakiwa hapa shuleni hivyo wanafunzi huishi maisha magumu na wengine huleta usumbufu kwa shule kwa kufikiri kuwa shule ina utaratibu wa kuwa na fedha kitu hicho hakipo ni jukumu lako mzazi/mlezi kumpa fedha za mahitaji yake kupitia simu ya shule.

b) Baadhi ya wanafunzi wamekuwa na tabia ya kukataa, kufanya kazi za nje kama usafi wa bweni, kufyeka n.k. shule haitavumilia tabia hiyo. Shule haitakuwa na huruma kwa mwanafunzi wa aina hii. Mwanafunzi lazima afundishwe Elimu ya kujitegemea. Na hii ndio sera ya taifa letu atafanya kazi zote za shule.



Edit with WPS Office

c) SIMU, ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu shuleni na kutumia vifaa vya muziki na camera shuleni. Mawasiliano yote ni kwa kupitia shule kwa namba tulizoorodhesha. Ni vizuri ukalielewa hili vizuri na hatutakuwa na huruma katika suala hili.

d) Vipodozi haviruhusiwi kabisa shuleni na ni kosa kisheria.

e) Usifike bwenini bila kuripoti ofisi ya Mkuu wa shule au Makamu mkuu wa shule.

f) Bank paying-slips ziwasilishwe kwa mhasibu wa shule mara tu ufikapo shulenina si vinginevyo. Hakikisha unapewa stakabadhi. Ahadi za kulipa baadaye hazitasikilizwa.

g) Vazi la shule lazima livaliwe wakati wote wa masomo na kwenye shughuli rasmi. Mavazi ya nyumbani hayaruhusiwi kabisa uwapo shuleni.

h) Maagizo ya fedha (karo na michango yote) na mahitaji yote muhimu vyote vitakaguliwa mara tu mwanafunzi atakapofika kujiunga na shule hii, visipokamilika mwanafunzi atarudishwa nyumbani kuvifuata.

i) Ni marufuku kuja na kofia, pete na mapambo mengine au mitindo isiyofaa ya kunyoa nywele.

j) Hairuhusiwi kufuga nywele, muda wote nywele ziwe fupi. Shule inayo saloon.

k) Ikiwezekana mfungulie Akaunti NMB au atafungua akiwa hapa shuleni kwa kushirikiana na Benki ya NMB au CRDB Makete.

l) Hatutaruhusu mwanafunzi kubaki wakati wa likizo hakikisha mzazi unatuma nauli mapema, sababu ni kwamba chakula cha kuwalisha wanafunzi hakipo wakati wa likizo.

8. AFYA: Unatakiwa kupima afya yako kabla ya kuripoti shuleni, fomu maalum imeambatanishwa kwa ajili hiyo na utatakiwa kukabidhi fomu hiyo iliyokamilika mara tu ufikapo shuleni.

Kama una matatizo ya muda mrefu ya kiafya toa taarifa ufikapo shuleni. Vyeti ni lazima uje navyo kama una matatizo sugu. Shule haina uwezo wa kutoa chakula maalum cha wagonjwa wakudumu. Shule haitavulimilia mwanafunzi anayejisingizia ugonjwa kwa sababu zake binafsi. Fomu ya daktari itatumika katika maamuzi yote.

Mwanafunzi aje na Bima ya Afya kama anayo, ambaye hana anashauriwa kujiunga kwenye Bima za kikaya CHF kwa mwaka.NB BIMA HIZI NI LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI

9. UHURU WA KUABUDU

Utaruhusiwa kuabudu kwa kadri ya dini kwa kufuata sheria, ratiba na taratibu za shule na za nchi, ingawa tabia ya kubughudhi wengine haitavumiliwa. Ukitaka kubadili dini ukiwa shuleni utatakiwa kuleta uthibitisho wa barua kutoka kwa mzazi wako. Shule yetu ni ya mchanganyiko pia kumbuka serikali haina dini hivyo shule haitakubali kuleta taratibu ili kubugudhi wengine.

10. KUBADILI JINA

Hautaruhusiwa kubadili jina lako litatakiwa kutumika kama lilivyotumika wakati wa mtihani wa kidato cha nne (4) au kama lilivyo kwenye Sel-form yako. Ili kupunguza usumbufu wa usajili katika kipengere hiki mwanafunzi anaporipoti anatakiwa kuja na nakala halisi na si copy ya cheti. Result Slips (origin).


11. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

a) Wizi
b) Kutohudhuria masomo zaidi ya siku 90 (utoro) bila taarifa.
c) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzie, walezi na wakubwa
d) Kugoma na kuhamasisha mgomo e) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi au kumpiga mwalimu



Edit with WPS Office

f) Uasherati na kujihusisha na mapenzi hapa shuleni na nje ya shule
g) Kuoa au kuolewa
h) Kutembelea majumba ya starehe guest house au hosteli ya wasichana/au wavulana
i) Ulevi/madawa ya kulevya (kutumia) au kukutwa nayo.
j) Kudharau bendera ya Taifa.
k) Kumiliki simu ya mkononi shuleni. l) Kuharibu mali za shule kwa makusudi au kuuza mali za shule.
m) Kugoma kufanya kazi halali za shule ambazo ni kwa manufaa yao na ustawi wao hapa shuleni.
n) Kuondoka shule kabla ya muda halali wa serikali na kutohudhuria Baraza la kufungia shule.
o) Kujihusisha na mapenzi ya jinsi moja.




ABKSA JOHN NGWALE

Nakala Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
S.L.P 06
Makete,

NB: Matibabu ya mtoto ni jukumu la mzazi na si la shule.

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.
SHULE YA SEKONDARI LUPILA

FOMU YA MAPATANO/KUKUBALI NAFASI YA MASOMO NA KUSOMA KATIKA SHULE HII KIDATO CHA __________ MWAKA__________

NB: Kabla ya kusaini soma kwa makini maagizo yote kama hutaridhika basi usifike kabisa. Tafuta shule yoyote Tanzania. Shule haitasikiliza vizingizio vya aina yoyote. pia kama afya yako si nzuri fanya utaratibu na mzazi wako kupata shule nyingine ukiwa huko huko shule haitataka usumbufu wowote. Au KAMA unataka masomo ambayo shule hii hayapo wasiliana na wizara ili ubadilishwe huko huko.

JINA LA MWANAFUNZI ____________________________________________
ANWANI:__________________________________________________________
MIMI_____________________________________________________________

Nimekubali/sikubali kujiunga na Jamuiya ya shule ya sekondari LUPILA. Nimesoma maagizo ya shule kwa makini na kuyaelewa Naahidi kuwa mtiifu na nitazingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Kinyume chake hatua kali zitachukuliwa dhidi yangu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Naahidi kusoma kwa bidii sana masomo yangu na kufaulu mitihani itakayotolewa na shule, Mkoa na Taifa.

Sahihi ya mwanafunzi__________________________ Tarehe__________________________________

B. Mzazi/mlezi

Mimi nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa kwa mtoto wangu nimekubali /sikubali mwanangu achukue nafasi hiyo. Naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na kitabia, Naahidi pia kumlipia karo ya shule/fedha za matibabu/na michango mingine mbalimbali iliyoagizwa na shule kwa wakati mwafaka kinyume chake nichukuliwe hatua za kisheria.

Sahihi ya mzazi /mlezi ________________________Tarehe__________________



Edit with WPS Office

NB: Fomu hii itawekwa kwenye faili au jalada lake.

Andika namba ya simu ya mzazi/Mlezi tu ____________ kwa ajili ya mawasiliano na shule.

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

LUPILA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 602
NJOMBE
DATE____________

TO THE MEDICAL OFFICER.

________________

________________


________________

PART A: Mr/Mrs/Miss____________________________________

Please examine the above named pupil as to her/his physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following categories.

1. Hemoglobin: ____________________________________
2. P.V. bleeding: ____________________________________
3. Eye sight: ____________________________________
4. Blood pressure: ____________________________________
5. Urine for sugar: ____________________________________
6. Stool for routine examination: ____________________________________
7. Skin, Diseases: ____________________________________
8. Asthma: ____________________________________
9. Leprosy: ____________________________________
10. Epilepsy: ____________________________________
11. Any deformity: ____________________________________
12. Pulmonary tuberculosis: ____________________________________
13. Neurosis: ____________________________________
14. Venereal Diseases: ____________________________________
15. Other serious Diseases: ____________________________________

Thank you




*ABKASA JOHN NGWALE*

(TO BE COMPLETED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)

1. I have examined the above named pupil and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for full time schooling. OTHER COMMENT:______________________________ 2. Date:__________Name and Signature__________________ Designation¬__________ __________________ Official Stamp__________



Edit with WPS Office

KIAMBATANISHO



Edit with WPS Office





Edit with WPS Office



Edit with WPS Office




Edit with WPS Office